

**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**

SHULE YA SEKONDARI VIDUNDA,  
S.L.P. 91,  
**KIDATU.**

**Tarehe.....**

**KUMB. NA.VDSS/SA/**

JINA LA MWANAFUNZI \_\_\_\_\_  
S.L.P. .....

---

**YAH: MAAGIZO KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI VIDUNDA WILAYA YA KILOSA  
MKOA WA MOROGORO MWAKA 2021**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukualifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Vidunda ipo umbali wa km 5, kutoka barabara kuu iendayo Ifakara, usafiri wa pikipiki kutoka Kidodi unapatikana katika kituo cha afya Kidodi, nauli ni T.Shs. 3,000/=. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021.

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia:**

**2.1 SARE ZA SHULE**

**(a) WAVULANA**

- Suruali mbili (2) za rangi ya bluu bahari na shati mbili (2) nyeupe tetroni mikono mifupi
- Viatu kisigino kifupi rangi nyeusi jozi mbili, soksi nyeupe jozi mbili na mkanda wa kiunoni mweusi wa ngozi,(mkanda wa utambi hauruhusiwi kabisa).
- Tai ndefu rangi ya kitambaa cha suruali

**(b) WASICHANA**

- Sketi mbili (2) za rangi ya bluu bahari na shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi.
- Viatu kisigino kifupi rangi nyeusi jozi mbili, soksi nyeupe jozi mbili.
- Tai ndefu rangi ya kitambaa cha sketi

**NB:** Kwa wasichana pindo la sketi kiuno liwe (1.5 inchi) Inchi moja na nusu.aidha viatu maarufu bajaji haviruhusiwi kabisa.

**(c)** Rangi ya Hijabu ifanane na sare ya shule (nyeupe) na ishonwe kubwa kufikia kwenye mikono.

**(d)** Tshirt za shule ambazo huvaliwa kwenye shughuli mbalimbali za shule hupatiakana

Shuleni kwa Tsh. 15,000/= ( Tshirt mbili)

- (d) Sare ya michezo kwa shule hii ni \_\_\_\_\_  
- Wavulana \_\_\_\_\_  
- Wasichana \_\_\_\_\_
- 2.2 Daftari tisa (9) (Counter book), kalamu za kutosha na mkebe wa hesabu.
- 2.3 Chakula cha wanafunzi , pamoja na matibabu ni gharama ya mzazi.
- 2.4 Mahitaji mengine ya kibinadamu kama usafi, vifaa vya kina mama.
- 2.5 Anatakiwa aje na 1. ....  
2. ....  
3. ....

3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii ni:-

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu No. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria No. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya ELimu Teknolojia na inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Rais Utumishi Tamisemi na utawala bora yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b. Mahudurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
- d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
- f. Kutunza usafi wa mwili na malazi na mazingira ya shule.
- g. Kuvala sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- i. Kutunza mali za Umma

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ufukuzwe shule.

- a. Wizi wa aina ye yote ile.
- b. Uasherati, ubakaji na ushoga
- c. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
- d. Uvutaji sigara na bangi
- e. Makosa ya jinai

- f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
  - g. Kudharau Bendera ya Taifa
  - h. Kuoa au kuolewa
  - i. Kupata mimba au kushawishi kutoa mimba
  - j. Kutoa mimba au kushawishi kutoa mimba
  - k. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani au usalama wa shule au watu.
  - l. Kukataa adhabu kwa makusudi
  - m. Kuwa na simu ya mkononi.
- 4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa na wanafunzi shulenii
- a. Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shule.
  - b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fupo na makosa ya jinai, form hii nayo utaikabidhi kwa mkuu wa shule.
  - c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
- 5.0 Tafadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu  
**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**

.....  
**SEBASTIAN B. KAPUNGA**

**MKUU WA SHULE**

**0677783436/0786166650/0753026165**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA  
SHULE YA SEKONDARI VIDUNDA**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA  
SHULE ULIYOPEWA**

Bandika picha  
hapa  
(Passport  
yenye shati  
jeupe)

**A: TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

- Jina kamili la mwanafunzi .....
- Tarehe ya kuzaliwa: .....(ambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa)
- Mahali ulipozaliwa .....
- Uraia .....
- Shule uliyotoka: .....
- Namba ya mtihani: Ps .....

**B: TAARIFA YA MZAZI/MLEZI**

- Jina la Mzazi/Mlezi: .....
- Kazi ya Mzazi/Mlezi: .....
- Anuani ya mzazi/mlezi: .....
- Namba ya simu ya mzazi/mlezi: .....

**C: MWANAFUNZI**

Mimi .....nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote kwa hiyo nakubali kuipokea nafasi niliyopewa. Ninaahidi kufuata sheria na taratibu za shule na kujifunza kwa bidii.

Saini: .....

Tarehe: .....

**D: MZAZI/MLEZI**

Mimi ..... Nimehakikisha mwanangu amezisoma na kuzielewa sheria na taratibu za shule na nimemesisitiza katika hilo. Pia naahidi kutokuwa kikwazo kwa mwanangu katika kujipatia Elimu yake.

Saini: .....

Tarehe: .....

**KUMBUKA: Fomu hii ijazwe kwa umakini na irudishwe shulenii mwanafunzi anaporipoti.**

**PRESIDENT'S OFFICE  
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**KILOSA DISTRICT COUNCIL  
VIDUNDA SECONDARY SCHOOL**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**FROM:** The Medical Officer  
Government Hospital .....  
.....  
.....  
.....

**To:** The Headmaster,  
Vidunda Secondary School,  
P.O.Box 91,  
**KIDATU.**

**RE: MEDICAL CERTIFICATE  
(TO BE COMPLETED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)**

I have examined ..... Who aspires to join form one (I) in your school as follows:

<b>AREA</b>	<b>REMARKS</b>
1. Skin	.....
2. Eyes	.....
3. Ears	.....
4. Teeth	.....
5. Chest	.....
6. Spleen	.....
7. Abdomen	.....
8. Urine	.....
9. Tool	.....
10. HB Haemoglobin	.....
11. Sickle cell	.....
12. Asthma	.....
13. Pregnancy for Girls	.....
14. Any other comments	.....
	.....

I consider that he/she is physically / not physically fit to join your school due to .....

Signature: ..... Date: ..... Official Stamp: .....